

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUSITISHA UZALISHAJI, UINGIZAJI KUTOKA NJE, USAMBAZAJI, UUZAJI NA MATUMIZI YA POMBE KALI ZILIZOFUNGASHWA KATIKA MIFUKO YA PLASTIKI (VIROBA)

1. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), pamoja na mambo mengine ina jukumu la kudhibiti usalama na ubora wa chakula ili kulinda afya ya jamii.
2. Mnamo tarehe 16/02/2017, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa alitoa agizo la kusitisha uzalishaji, uingizaji kutoka nje, usambazaji, uuzaji na matumizi ya pombe kali zinazofungashwa kwenye vifungashio vya plastiki (viroba) kuanzia tarehe 01 Machi, 2017.
3. Kwa kuzingatia agizo hilo na Kanuni za Kukataza Uzalishaji, Uingizaji na Matumizi ya Vifungashio vya Plastiki kufungashia Pombe kali za mwaka 2017 (*The Environmental Management (Prohibition of Manufacturing, Importation and Use of Plastic Sachets for Packaging Distilled and other alcoholic beverages) Regulations 2017*), imekatazwa kutumia vifungashio vya plastiki (sachets) kufungashia pombe kali. Badala yake wazalishaji watapaswa kufungasha pombe kali hizo katika chupa zenye ujazo usiopungua mililita 200.
4. Ikiwa ni sehemu ya jukumu la udhibiti wa usalama wa vyakula, mpaka kufikia tarehe 1 Machi, 2017 TFDA ilikuwa imesajili matumizi ya aina 20 za vinywaji vya pombe kali vilivyofungashwa katika mifuko ya plastiki ikiwa ni pamoja na aina tano ambazo muda wa usajili umekwisha. Usajili huu hutolewa baada ya kujiridhisha na usalama wake pamoja na masharti mengine ya kisheria.
5. Uamuzi wa Serikali wa kupiga marufuku matumizi ya pombe za aina hiyo unatokana na athari mbalimbali ikiwa ni pamoja na za kiafya na kijamii. Matumizi mabaya ya pombe hizo yamesababisha ajali nyingi, vifo, ulemavu na mzigo mkubwa kwa Serikali wa kutoa huduma za tiba na ongezeko la makosa ya jinai. Aidha, kutokana na teknolojia rahisi ya utengenezaji wa aina hizo za pombe, imekuwa rahisi kwa baadhi ya watu kutengeneza vinywaji bandia ambapo kuna uwezekano mkubwa wa kutengeneza vinywaji ambavyo si salama kwa hiyo kuathiri afya za watumiaji.
6. Ili kutekeleza maelekezo ya Serikali kwa ufanisi, napenda kuutaarifu umma kuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kuanzia tarehe 01 Machi, 2017 imechukua hatua kama ifuatavyo:-
 - (a) Kufuta usajili, vibali vya uzalishaji, uingizaji kutoka nje ya nchi, uambazaji, hifadhi na uuzaji wa vinywaji vya pombe kali ambazo zimefungashwa katika mifuko ya plastiki (sachets) na chupa za plastiki zenye ujazo chini ya mililita 200 kwa mujibu wa Kifungu cha 25(1) cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219. Aidha, matumizi ya

pombe za aina hiyo hazina tija kwa taifa kwa mujibu wa kifungu 20(2)(b)(2) cha Sheria hiyo; na

- (b) Kusitisha upokeaji wa maombi mapya ya usajili au vibali vya utengenezaji, uingizaji kutoka nje ya nchi, usambazaji, hifadhi na uuzwaji wa vinywaji vya aina hiyo hayatapokelewa na TFDA.
7. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto inaendelea kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Serikali kuhusu suala hili ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, napenda kusesitiza kwa wafanyabiasha na wananchi wanaojihusisha na biashara ya vinywaji na matumizi ya pombe kali za aina hiyo kutii maelekezo ya Serikali mara moja ili kujiepusha na hatua zaidi kuchukuliwa dhidi yao.
8. Mwisho, Wizara inatoa rai kwa kila mwananchi kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa maelekezo ya Serikali kwa kutoa taarifa zitakazoweza kubaini wale wote wanaokaidi agizo hili la Serikali ili kulinda afya na ustawi wa jamii.

Imetolewa na;

UMMY MWALIMU (MB)
WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO
TAREHE 21 MACHI, 2017